

SchoolCash Online

SchoolCash Online Ni Nini?

SchoolCash Online ni njia rahisi na salama kutumia ya kulipa ada ya shule ya mwanafunzi wako. Unaweza kulipia ziara za darasa za mwanafunzi wako na mengineyo kwa mibofyo michache.

Jinsi ya kujiandikisha katika SchoolCash Online

HATUA YA 1:

- Nenda kwenye ukurasa wa SchoolCash: <https://www.schoolcashionline.com/>
- Bofya chaguo la Jiandikishe.
- Utaelekezwa kwenye ukurasa wa Kujiandikisha kwa Mtumiaji
- Jaza fomu ya Kujiandikisha kwa Mtumiaji.

Kidokezo: Nenosiri lako lazima liwe na angalau herufi 8, herufi moja kubwa, herufi moja ndogo na namba moja.

Kumbuka: x nyekundu inaonyesha kuwa kuna hitilafu kwenye maelezo uliyoweka. Jaza sehemu zote ambazo hazina tiki ya bluu na nyeupe upande wa kulia.

Chagua Endelea.

Utaelekezwa kwenye ukurasa wa Barua Pepe ya Kuthibitisha.

HATUA YA 2:

- Angalia kikasha chako cha barua pepe ili uone barua pepe kutoka noreply@schoolcashionline.com.
- Bofya kiungo cha Uthibitishaji wa Kujiandikisha.
- Kichupo kipya kitafunguka cha kukufahamisha kuwa umejiandikisha.

Muda: School Cash Online: Thibitisha Anwani Yako ya Barua Pepe
Kwa: Jane00e
Kutoka: noreply@schoolcashionline.com
Ilipokewa: Ijumaa Tarehe 24 Januari 2020 Saa 14:29:55 GMT-0500 (Eastern Standard Time)
Anwani ya IP Iliyotuma: html
Sehemu: html
Viambatisho

Hujambo Jane,

taadhi bofya kiungo kiticho napa chini ili uthebitishe anwani yako ya barua pepe.

<https://www.schoolcashionline.com/Registration/Confirm/ConfirmationEmail/1b2e1f43-963b-4515-e775ef5c-556a>

Idwa kiungo hakifanyi kazi, nakili kiungo hicho na ukibandike kwenye kwinjari chako.

Asante,

Timu ya Usaidizi wa School Cash Online



HATUA YA 3

- Weka Mwanafunzi: Chagua bodi ya shule yako (Halifax Regional Centre for Education), chagua shule yako (Rocky Lake Elementary).
- Weka jina la kwanza la mwanafunzi wako, jina la mwisho na tarehe ya kuzaliwa

Umemaliza kufungua akaunti na uko tayari kununua bidhaa!

MASWALI YANAYOULIZWA SANA

- **Ninawezaje kupata kitambulisho cha mwanafunzi wangu?**

Unaweza kupata kitambulisho cha mwanafunzi kwa kuwasiliana msimamizi msaidizi, jsheldon@hrce.ca

- **Sipati bidhaa ambayo ningependa kununua**

Ingia katika Akaunti, chagua kichupo cha Bidhaa. Utaona vichupo vidogo tofauti, ikijumuisha majina ya wanafunzi wako, jina la wilaya ya shule na Onyesha Bidhaa Zote. Chagua kichupo kidogo ambacho ungependa kuangalia bidhaa zake. Mfano. Jina la mwanafunzi. Ikiwa huoni bidhaa ambayo ungependa kununua, tafadhali wasiliana na msimamizi msaidizi wa shule yako.

Sababu za kukosekana kwa bidhaa zinajumuisha kusahaulika kimakosa, kuisha kwa muda wa bidhaa, kuisha kwa bidhaa, bidhaa bado haijawekwa na bidhaa hiyo tayari ilikuwa imenunuliwa kwa mwanafunzi huyo.

- **Kurejeshewa pesa**

Ili kuomba kurejeshewa pesa kwa bidhaa uliyonunua kwenye SchoolCash Online, wasiliana na mfanyakazi msimamizi wa shule.